BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KUPITIA RIPOTI YA KAMATI YA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Mheshimiwa Spika, naomba kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutujaalia Uhai na Afya njema ambayo imetuwezesha kutekeleza vyema majukumu yetu ya kila siku. Vile vile, nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika pamoja na wasaidizi wako kwa mnavyosimamia chombo hiki kwa uadilifu wa hali ya juu ili kufikia malengo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi pamoja na Mipango mbali mbali ya Kitaifa katika kukuza Demokrasia.

Mheshimiwa Spika, pia, sina budi kumshukuru Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa uongozi wake wenye mashirikiano makubwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Harous Said Suleiman kwa uwezo na busara zake ziliomfanya apate mafanikio makubwa katika Ofisi hii pamoja na kuwapongeza watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Omar Dadi Shajak kwa mashirikiano yao

wanayotupatia wakati wa shughuli zetu za kil asiku za Kamati kwani bila wao Kamati isingeweza kutimiza malengo yake.

Mheshimiwa Spika, aidha, nitumie fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kwa namna wanavyoweza kutekeleza wajibu wao wa kujadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali ambayo yametolewa ufafanuzi na Ofisi hii kwa lengo la kuhakikisha kwamba utekelezaji wa maoni/ushauri na mapendekezo yaliotolewa ndani ya ripoti ya Kamati yetu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 chini ya Taasisi zake; utekelezaji wake umekuwa ni chachu ya maendeleo kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza lakini pia, katika kukuza na kuendeleza maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima naomba sasa uniruhusu kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Machano Othman Said	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mussa Foum Mussa	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Abadalla Abass Wadi	Mjumbe
4.	Mhe. Haji Shaaban Waziri	Mjumbe
5.	Mhe. Maryam Thani Juma	Mjumbe
6.	Mhe. Zaina Abdalla Salum	Mjumbe
7.	Mhe. Mwanaisha Mohammed Kheir	Katibu
8.	Nd. Ali Alawy Ali	Katibu
9.	Nd. Shawana Mohammed Haji	Katibu
10.	Nd. Amina Abeid Hemed	Mkalimani

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia Kanuni ya 107(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la 2020 Kamati zimepewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia; ambapo kazi hii ilifanywa vyema kwa kipindi hiki kilichopita na bado Kamati inazidi kufuatilia utekelezaji wa maoni hayo kila inapoona inafaa kufanya.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kanuni ya *109(17)* ya Kanuni za Baraza, inaelezea kuwa kabla ya kuwasilishwa Barazani utekelezaji wa maoni na ushauri huo, Kamati inatakiwa kukaa na wizara husika ili kujadili utekelezaji huo unaojumuisha maoni na ushauri uliotolewa na Kamati dhidi ya wizara na taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, Hotuba hii inaunga mkono utekelezaji wa maoni ya Kamati na inaelekeza kuwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imejitahidi kwa kiasi kikubwa katika kutekeleza majukumu hayo licha ya changamoto ndogo ndogo ambazo kimsingi utatuzi wake unafanyiwa kazi. Hata hivyo, jumla ya maoni na ushauri kumi na saba (*17)* yaliagizwa katika Taasisi mbali mbali kupitia ripoti ya Kamati katika mwaka wa fedha 2022/2023 na jambo jema ni kuwa maoni hayo yamepatiwa majibu kutokana na utekelezaji wake ambao hadi sasa unaendelea. Aidha, Kamati inatoa ufafanuzi mchache kuhusiana na baadhi ya hoja za maoni na ushauri uliotolewa kutokana na namna utekelezaji wake ulivyoibuka katika mjadala mbele ya Kamati.

Utekelezaji wa Mapendekezo, maoni na ushauri wa Kamati kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

a) **Mamlaka na Idara ya Mazingira Zanzibar**

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati yetu imeridhishwa na utekelezaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati kupitia ripoti yetu ya mwaka jana, isipokuwa kutokana na changamoto mbali mbali zinazoikabili Ofisi hii kupitia Taasisi zake, tunaiomba Serikali kuzidisha kasi katika kuzisaidia Taasisi Programu zao kutekelezwa kwa kuziondoa changamoto kadhaa zinazoikabili Ofisi hii.

Hoja Namba 1

"Kamati ilipata fursa ya kutembeela maeneo yaliyoathirika zaidi na mabadiliko ya Tabianchi ambayo ni Tovuni, Sipwese, Likoni, Kichanjaani Ndagoni na Mikindani Mtwara. Kamati imeridhishwa na miradi hii na hivyo, tunaishauri Serikali kuhamishia nguvu zake za uhifadhi wa mazingira katika eneo la Kichanjaani, Shehia ya Ndagoni."

Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu ya utekelezaji wa hoja hii, Kamati yangu imeitaka Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuonesha mipango na mikakati mbali mbali waliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na kubainisha kipindi ambacho mipango hiyo imepangwa kutekelezwa. Lengo na ushauri huu ni kuweka wazi utekelezaji wa agizo hili na kuifanya jamii ione jitihada zinazochukuliwa dhidi ya eneo husika.

Hoja Namba 3

"Kamati inaendelea kushauri kufanyiwa mapitio ya Sheria zote zinazohusiana na mazingira kama vile Sheria ya Misitu na Sheria ya Usafiri Baharini na kutunga Sheria mpya ya Madini itakayojumuisha, pamoja na mambo mengine, usimamizi wa maliasili zisizorejesheka."

Mheshimiwa Spika, Kamati imeelezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Ofisi ya Makamu wa Kwanza imepanga kufanya mapitio ya Sera ya Mazingira ya mwaka 2013 ambapo tarehe 21/8/2023 Ofisi ilisaini mkataba wa makubaliano na Taasisi ya Serikali iitwayo *Climate Action Network Tanzania* juu ya utayarishwaji wa Sera mpya ya Mazingira pamoja na mkakati wa mabadiliko ya Tabianchi. Baada ya kufanywa marekebbisho hayo ndio Ofisi ya Makamu wa Kwanza itafanya marekebosho ya Sera yake ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2015. Hata hivyo, Kamati inaitaka Ofisi kuwasiliana na Taasisi zote husika na kuzishauri namna ya kubuni mikakati itakayosaidia kupata Sera mpya inayoendana na mahitaji ya Sera na Sheria mpya ya Madini hapa Zanzibar.

Hoja Namba 5

"Serikali izidishe kasi ya mapambano dhidi ya uingizaji, usambazaji na matumizi ya mifuko ya plastiki kwa taasisi zinazohusika kuwachukulia hatua za kisheria wahusika…"

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imeridhika na juhudi za kupunguza matumizi ya mifuko ya plastiki ambapo tumekuwa tukiona na kusikia vipindi mbali mbali katika vyombo vya habari vikielezea changamoto ya mifuko hii katika mazingira. Sambamba na hayo, Kamati imeitaka Ofisi kuainisha katika ripoti yake ni operesheni ngapi zilifanyika ndani ya mwaka 2022/2023 na wahusika wangapi walichukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria za nchi. Aidha, Ofisi inatakiwa kueleza msimamo wa Serikali kuhusiana na matumizi ya vifungashio vya plastiki ambavyo vinatumika kupitia bidhaa mbali mbali za majumbani ikiwemo chupa za maji.

b) Tume ya UKIMWI Zanzibar

Hoja Namba 1

"…Ofisi kwa kushirikiana na NGO's ziendelee kutoa uelewa na kuihamasisha jamii kupitia mitandao ya kijamii, redio, televisheni na mikutano juu ya uwepo wa maradhi ya UKIMWI na athari zake kwa jamii na uchumi wetu kwa ujumla."

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Tume ya UKIMWI inaendelea kutoa elimu kwa kutumia njia mbali mbali, sambamba na kutumia mitandao ya kijamii ili kuwafikia walengwa walio wengi ambao ni rika la vijana. Kwa juhudi hizi, Kamati yangu inaipongeza Tume ya UKIMWI Zanzibar kwa kutekeleza vyema ushauri wa Kamati na kuitaka Tume kuzidi kutoa elimu kwa umma ya kuiasa jamii kuwa ugonjwa huu bado upo na unaiyathiri jamii katika harakati zake za kila siku. Sambamba na hilo, Kamati bado inaitaka Serikali kuwapatia Tume ya Ukimwi fungu kubwa la fedha ili kuendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali juu ya tatizo la ukimwi.

c) Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar:

Hoja Namba 2

"Mashirikiano zaidi yajengwe baina ya jamii na Mamlaka ili kusaidia kupata taarifa za kudhibiti bandari bubu ambazo inasemekana kwa kiasi kikubwa zinatumika kupitishia dawa za kulevya kwa pwani ya Zanzibar."

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupiti Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imeweka mikakati ya kukuza

mashirikiano na jamii ikiwemo kufanya mikutano ya wazi na wanajamii. Kamati haina pingamizi na utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka hii kwani ndio kiungo muhimu cha kupinga matendo ya uharamia unaosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya nchini. Hata hivyo, Kamati inasikitishwa na kuona kwamba bado jamii haijaonyesha utayari wa kuendeleza mapambano haya na wapo baadhi ya wananchi wanakataa hata kusaidia kutoa ushahidi dhidi ya wahalifu.

Hoja Namba 5

"Kamati inaishauri jamii kujenga mazoea ya kuwaona waathirika wa dawa za kulevya kuwa ni watu wema na wenye kuaminiwa katika jamii baada ya kutoka vituoa vya kurekebisha tabia."

Mheshimiwa Spika, Katika utekelezaji wa agizo hili, Mamlaka imeendelea kutoa elimu kwa umma kupitia programu ya kuwaunganisha waathirika wa dawa za kulevya baada ya kupata tiba inayolenga kuifanya jamii iwapokee na kuwapa mashirikiano mema waathirika hao.

Sambamba na hayo, Kamati imezidi kuishauri Serikali kuhusu kukamilisha mpango wa ujenzi wa kituo cha Kidimni Unguja na vile vile, kuanza maandalizi ya ujenzi wa kituo kipya kwa upande wa Pemba ili kuweka mazingira bora ya kutolea huduma kwa waathirika wa dawa za kulevya. Kukamilika kwa mpango wa ujenzi wa kituo cha Kidimni na Kangagani Pemba kutapunguza au kuondosha kabisa vituo binafsi ambavyo vinakuwa na changamoto nyingi katika kuwahudumima waathirika.

Mheshimiwa Spika, Mwisho wa hayo, Kamati inapenda kuchukuwa fursa hii kuishauri jamii kutoa mashirikiano na Mamlaka ya Mazingira kwa kudumisha usafi

na uhifadhi wa mazingira kwa kupinga matumizi yasiyo sahihi na kutoa taarifa pindi tu watakapo baini kuwepo kwa uharibifu wa mazingira katika maeneo yao. Aidha, Kamati inaiyomba jamii kuunga mkono juhudi za Serikali katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya, mapambano dhidi ya gonjwa la UKIMWI pamoja na kuiasa jamii kutojishirikisha na vitendo vyote viovu ambavyo vinaharibu haiba, mila na silka ya wazanzibari.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, napenda kutumia tena nafasi hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni haya na kwa niaba ya Kamati yangu pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kuwa watulivu na kunisikiliza muda wote wa kuwasilisha hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ***Naomba Kuwasilisha.***

Ahsante,



(Mhe. Machano Othman Said)

Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

BARAZA LA WAWAKILISHI

ZANZIBAR